

Maswali

1. Sema sababu mbili zilizomfanya Yesu atende miujiza?
2. Yule mtu aliyeletwa kwa Yesu alikuwa na shida gani?
3. Mbona Mafarisayo walikuwa hapo?
4. Mbona ilikuwa vigumu sana huyo mgonjwa kufikia Yesu?
5. Walifanya nini ndiyo wamfikie Yesu?
6. Mwanzoni Yesu alimwambia nini mgonjwa?
7. Mafarisayo walifikiria nini juu ya huyo mtu?
8. Yesu alifanya nini kuwaonyesha ana uwezo wa kusameha dhambi?

Majibu

1. A). Alipenda watu; B). Alitaka kuonyesha kwamba yeye ni Mwana wa Mungu.
2. Alipooza.
3. Mafarisayo walikuwa hapo kumfanyia Yesu hila ili atende kinyume na sheria.
4. Ilikuwa vigumu kumfikia Yesu kwa sababu watu walikuwa wengi.
5. Walitumia vipandio mpaka wakafika kwa paa. Walichimba paa na kupenya mwanya waliyoiteremshia mgonjwa kwa mkeka.
6. Yesu alisema, “Umesamehewa dhambi zako.”
7. Mafarisayo walichukizwa kwa sababu waliamini kwamba ni Mungu tu anaweza kusamehe dhambi.
8. Yesu aliponya mtu aliyepooza hata akaamka, akatembea na kwenda nyumbani.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



38 Kuponya mtu aliyepooza

Marejeo

Luka 5:17—26

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Yesu alikuwa na uwezo wa kusamehe watu dhambi na kuwaponya magonjwa yao.

Maneno maalum

1. Sababu ya miujiza + upendo
2. Nyumba inamsongamano + mafarisayo +pooza + amini
3. Mpango + hatua + paa
4. Mishipi + lima + jua inakausha
5. Kwaruza + shimo + teremsha
6. Sameha dhambi + mtu anafurahi + Mafarisayo hawana furaha.
7. Ushahidi wa msameha + simama na uondoke + simama na kuondoka + shangaa

38.1 Tumejifunza kwamba Yesu kama mwana wa Mungu alifanya mengi yasioweza kufanywa na watu wa kawaida. Aliponya watu kwa sababu aliwapenda sana. Yesu hakutaka kukawakasirisha watawala, lakini alitaka kuonyesha watu wote waume kwa wake kwamba yeye ni Mwana wa Mungu. Hizi sababu mbili zilifanya Yesu atende miujiza.

38.2 Siku moja Yesu alikuwa kwa nyumba katika mji wa Kapernaumu akizungumza na watu wengi. Hawa watu wengi walikuwa kwa nyumba moja iliyokuwa na chumba kimoja tu. Kwa hivyo wengi walikuwa nje wamesimama mlangoni na hata kwa dirisha. Waliangalia waone nini ilikuwa ikiendelea. Wengine wao walikuwa Mafarisayo. Walikuwa hapo wakitafuta namna ya kumtega Yesu. Wakati Yesu alipokuwa akizungumza watu wanne walifika wamebeba mtu mgonjwa. Alikuwa amepooza na amebebwa kwa mkeka. Watu hawa walikuwa wamesikia habari ya Yesu na waliamini kwamba angeponya rafiki yao.

38.3 Walipofika walikuta umati wa watu wengi na wakaona kwamba haitakuwa raisi kumfikia Yesu. Badala ya kurudi na huzuni, waliamua kufanya tendo la ujasiri. Walienda kando ya nyumba penye kulikuwa na vipandio (daraja) vya kutumia kwenda juu ya paa. Walipanda mpaka juu. Haikukuwa raisi kwa vile walikuwa na mgonjwa aliyelala kwa mkeka. Walifika kwa paa na kuweka mgonjwa chini.



38.4 Walifunga kamba ya nguvu kwa kila pembe ya mkeka-labda zilikuwa mishipi ya joho (nguo) zao. Wakachunguza waone penye Yesu alikuwa halafu wakaanza kuchimba mwanya kwa paa. Pengine walipata vifaa vya kutumia. Nyumba za wakati huo zilikuwa kama za saa hii kwa nchi zingine-zilijengwa kwa udongo na kukauka. Kwa hivyo haikukuwa ngumu kuchimba shimo kubwa kwenye paa.

38.5 Mikwaruzo iliposikika kutoka juu yao Yesu aliacha kuzungumza. Waliangalia juu. Kulikuwa na shimo chini ya dari. Kidogo kidogo ikawa kubwa. Waliokuwa wakichimba walijaribu wasiangushe mchanga au vipande chini. Watu waliokuwa chini walianza kuona sura za watu waliokuwa juu. Bunde tu shimo lilikuwa kubwa la kutosha wale watu wanne wamteremshe rafiki wao kwa mkeka mpaka chini alikokuwa Yesu



38.6 Waliokuwa ndani ya nyumba waliacha nafasi ya kutosha ili wamueke yule mgonjwa aliyepooza sakafuni. Labda baadhi ya hao watu wengi walimjua. Yesu alimwambia mgonjwa, “Umesamehewa dhambi zako.” Huyu mtu hakutarajia kusikia hayo lakini kwa sababu aliamini Yesu, labda alifurahi. Mafarisayo hawakufurahi tena walichukizwa. Walifikiri kwamba ni Mungu tu ndiye anasameha dhambi.

38.7 Yesu alijua walichokuwa wakifikiri na akasema, “Mkitaka kujua kwamba Mwana wa mtu anauwezo wa kusameha dhambi, ninaambia huyu mtu simama chukua mkeka wako na uende nyumbani.” Papo hapo aliyekuwa amepooza alisimama akaenda amebeba mkeka wake. Alishukuru Yesu na kumsifu Mungu. Watu walimsongea ili apate nafasi ya kuenda. Walishangaa kwa kuona hayo.